# WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII

Mada :Hali ya Utoaji wa Huduma za Ustawi wa Jamii nchini 2014/2015

**Mwasilishaji** : Rabikira O. Mushi, Kaimu Kamishna wa Ustawi wa Jamii

Mkutano wa RMOs & DMOs Blue Pearl Dar Es Salaam.

# Utangulizi

Mada hii itazungumzia hali ya huduma za ustawi wa jamii katika maeneo makuu manne;

- Tathmini ya huduma za Ustawi wa Jamii nchini
- Huduma kwa familia na watoto
- Huduma ya haki za mtoto na marekebisho ya tabia
- Huduma kwa wazee na watu wenye ulemavu

# Tathmini ya Huduma za Ustawi wa Jamii nchini

- Katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara ilifanya tathmini ya Huduma za Ustawi Jamii nchini .Lengo lilikuwa ni kuangalia wigo wa watoa huduma na hali ya huduma hizo.
- Tathmini hiyo imebainisha changamoto, mafanikio na fursa mbalimbali.

# Uimara na fursa za utoaji wa huduma

- Huduma katika mahabusu za watoto 5 zilizopo ni za kuridhisha .
- Asilimia 98 ya halmashauri zina walau Afisa ustawi mmoja . Hii ni hatua kubwa kulinganisha na mwaka 2012/13 ambapo ilikuwa ni 75%.
- Kuna ushirikiano mzuri kati ya halmashauri na vituo vinavyotoa huduma za ustawi wa jamii.

# …..Uimara  na fursa za utoaji wa huduma

- Vituo vya ustawi wa jamii vina rasilimali ambazo zinaweza kutumika kwa kuingia ubia na ushirikiano na sekta binafsi.

# Changamoto

- Asilimia 54 ya vituo 298 vya watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi vilivyofikiwa vinaendeshwa bila leseni . Aidha vituo hivyo havina mpango wa malezi (care plan) hivyo kuwafanya watoto hao kuishi muda mrefu bila kutengamanishwa.
- Kuchakaa kwa miundo mbinu katika makazi ya Wazee na vyuo vya WWU.

# …inaendelea.

- Asilimia 46 ya vituo vya kulelea watoto wadogo mchana ya vituo 194 vilivyofikiwa vimesajiliwa .Aidha taarifa imebainisha kuwa maafisa ustawi wa jamii katika halmashauri hawafanyi ufuatiliaji wala ukaguzi wa vituo hivi.

# 1. Huduma kwa  Familia na Watoto

- **Huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa**

  Utulivu na amani katika ndoa ni jambo la msingi katika ustawi ,afya na maendeleo ya familia, jamii na taifa
- Katika kuimarisha mahusiano katika ndoa Idara ya ustawi wa jamii imeendelea kupokea mashauri na kutafuta ufumbuzi wa matatizo hayo.


# …inaendelea.

- Katika kipindi hiki jumla ya mashauri ya ndoa 11,922 yalishughulikiwa. Mashauri 4768 (40%) yalisuluhishwa na mengine 7154 (60%) yalipelekwa mahakamani kwa ufumbuzi wa kisheria.
- Migogoro hii inachangiwa na sababu mbalimbali ikiwemo umri wa wanandoa,hali ya kiuchumi , tabia na mienendo ya wanandoa husika.


# Inaendelea……

- Taarifa zinaonesha kuwa kundi rika linaloathiriwa zaidi na migogoro ya ndoa ni kundi la umri wa kati .
- Kundi hili ndilo ambalo linachangia kwa kiwango kikubwa katika maendeleo ya jamii na uchumi wa Taifa

# % Mgawanyo wa mashauri ya ndoa kulingana na umri .



# …Mchoro kuonesha sababu za migogoro katika ndoa.



# Athari za Migogoro ya ndoa.

- Migogoro ya ndoa ni chanzo cha magonjwa mbalimbali. Mfano UKIMWI,sonona n.k
- Matatizo mbalimbali ya kijamii mfano kujinyonga
- Kuongezeka kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi
- Kuongezeka kwa matukio ya ukatili wa kijinsia. Mfano Mkoa wa kagera umeripoti jumla ya matukio 312 kati ya 735 ya ukatili wa kijinsia kwa mwaka 2014/2015.

# Programu za Ulinzi na Usalama wa Mtoto

- Katika kipindi hiki Wizara iliendelea kuimarisha mifumo ya ulinzi na usalama wa mtoto
- Jumla ya halmashauri 32 ziliwezeshwa kuanzisha timu za ulinzi na usalama wa mtoto.
- Jumla ya wataalamu 815 walipatiwa mafunzo mbalimbali kuhusu namna ya kutoa huduma za ulinzi na usalama wa mtoto katika maeneo yao.

# ….Inaendelea

- Kwa mujibu ya Sheria ya Mtoto (2009) Kifungu cha 94 mamlaka za serikali za mtaa zina wajibu kuwalinda na kuwahudumia watoto katika maeneo yake . Pia kifungu cha 95 cha sheria hiyo kinampa wajibu kila mwanajamii kutoa taarifa za matukio ya unyanyasaji na ukatili kwa mamlaka husika bila kuchelewa.
- Kwahiyo,ni jukumu la Wajumbe wa RHMT na CHMT kuratibu na kutoa huduma stahiki za matunzo,tiba na za kisaikolojia kwa watoto waliofanyiwa ukatili .

# …inaendelea.

- Jumla ya matukio 3449 yaliripotiwa kwa mwaka 2014/15 kulinganisha na matukio 2250 yalio ripotiwa mwaka 2013/14 kutokana na kuimarishwa kwa mifumo ya ulinzi na usalama wa mtoto

# Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto

- Malezi na makuzi ya awali ya mtoto ni muhimu katika kumjenga mtoto kimwili, kiakili, kijamii, kimaono/kihisia na lugha.
- Katika kipindi hiki jumla ya vituo 24 vya kulelea watoto wadogo mchana vimesajiliwa na kufanya idadi ya vituo vilivyo sajiliwa kufikia 731.

# …Inaendelea

- Hata hivyo ,Mikoa mingi haiwasilishi maombi ya usajili wa vituo hivi. Ni mikoa 13 tu ndio imewasilisha maombi ambayo ni Arusha, Iringa, Morogoro, Mwanza, Ruvuma, Tanga, Pwani, DSM, Shinyanga, Kagera, Mtwara na Kilimanjaro.

Ni jukumu la maafisa Ustawi wa Jamii wa Sekretarieti za mikoa na Halmashauri kuhakikisha vituo vya watoto wadogo mchana vinaendeshwa kwa mujibu wa sheria.

# Malezi ya Kambo na Kuasili

- Wizara imeendelea kusimamia utoaji wa huduma ya malezi ya kambo na kuasili. Katika kipindi hiki jumla ya maombi 87 yalipokelewa .Kati ya maombi hayo watoto 48 wamepata huduma ya malezi ya kambo na watoto 29 wameasiliwa. Maombi 7 yalipelekwa kwenye taasisi ya kimataifa ya huduma za kijamii (ISS) kwa ajili ya taarifa za kiuchunguzi na ombi moja lilikataliwa kwa sababu ya kutokidhi vigezo

- Maombi mengi yanayowasilishwa yanatoka katika mikoa ya ; Dar es salaam, Mwanza, Arusha na Kilimanjaro . Aidha wananchi wengi inaonekana hawaelewi vema kuhusu huduma hii. Ni Jukumiu la Maafisa Ustawi wa Jamii kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa huduma hii .

# Makao ya watoto WKMH

- Wizara imeendelea kuratibu huduma za makao ya watoto nchini.
- Katika kuboresha utoaji wa huduma za makao ya watoto, mwaka (2014) Wizara ilitoa waraka ulioelekeza halmashauri kuimarisha huduma za makao ya watoto. Halmashauri za Meru, Temeke na Hai zimechukua hatua za kufunga

makao yanayoendeshwa kinyume cha sheria

# …inaendelea.

- Wizara inaelekeza maafisa ustawi wa jamii katika kufanya ufuatiliaji na ukaguzi wa mara kwa mara katika makao ya watoto yaliyoko katika maeneo yenu

# Huduma kwa Wakimbizi Mkoani Kigoma

- Katika kipindi hiki Wizara ilishiriki katika kutoa huduma za ustawi wa jamii kwa watoto na makundi mengine maalum katika kambi ya Wakimbizi Nyarugusu, mkoani Kigoma . Jumla ya maafisa ustawi wa jamii 45 wanashiriki katika zoezi hili.
- Huduma zilizotolewa ni kuwaunganisha watoto na wazazi/walezi wao, kuwapa hifadhi ya muda kwa walezi wa kambo,kuwapa rufaa ili kupata huduma za afya,unasihi,malazi na chakula

# …inaendelea.

- Hadi Agosti 15 jumla ya watoto 1435 walipatiwa huduma hizi .Kazi hii inaendelea hadi Septemba 2015 .

# Huduma za Haki ya Mtoto na Marekebisho ya Tabia

Wizara imeendelea kuratibu, kusimamia na kutoa huduma kwa watoto walio katika mkinzano na sheria, wanaokutana na mfumo wa sheria, watoto watukutu na watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani. Huduma hizi zinatolewa katika Mahabusu za watoto, shule ya maadilisho, vituo vya watoto wa mitaani; vizuizi( magereza na polisi) na katika jamii kwa ujumla.

# Huduma zilizotolewa

- Kuandaa Kanuni za Kamati za Ustawi katika Mahabusu za Watoto. Mafunzo yametolewa katika mahabusu tano(5)
- Watumishi wa Mahabusu za watoto na shule ya maadilisho waliwezeshwa kujua kanuni za sheria ya mtoto
- Kufanya mikutano ya uhamasishaji ya namna ya uanzishaji wa kamati za ustawi katika mahabusu za watoto kwa kamati za CMT, CHMT katika Jiji la Arusha, Tanga, Manispaa ya Ilala na Halmashauri ya Mbeya.

# Mpango wa Kuwachepua Watoto Walio katika Mkinzano na Sheria

- Wizara inatekeleza mradi wa kuwachepua watoto walio katika mkinzano na sheria ili wapate marekebisho nje ya mfumo rasmi wa kisheria.Mradi huu unatekelezwa katika Manispaa ya Temeke na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.
- Katika kipindi hiki jumla ya watoto 235 walichepushwa; Dar es Salaam Watoto 206 na Mbeya watoto 29.

# Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu na Wazee

- Wizara imekamilisha Mwongozo wa Utambuzi wa Mapema na Afua kwa Watoto Wenye Ulemavu .Mwongozo huu unalenga kuwatambua mapema watoto na kuwapa huduma za marekebisho kwa wakati

# ……inaendelea.

- Mwongozo huu ni nyenzo ya utaoaji huduma kwa maafisa ustawi wa jamii, watoa huduma za afya na elimu, wazazi,walezi wa watoto na jamii. Aidha utawawezesha wazazi/walezi kuweza kutambua ulemavu mapema kwa watoto hao na kuweza kuwapeleka katika huduma stahiki.

# …inaendelea.

- Mwongozo huu umefanyiwa majaribio katika Halmashauri za Shinyanga na Iringa ambapo jumla ya wataalamu 50 wamepatiwa mafunzo
- Mwongozo huu utaanza kusambazwa mwaka huu wa fedha.

# Huduma za utengamao kwa Watu Wenye Ulemavu

- Katika kipindi hiki Wizara imetoa mafunzo ya marekebisho na utengamao kwa maafisa ustawi wa jamii 10 kutoka katika Wilaya za Mvomero,Kilombero,Ruangwa,Dodoma ,Nkasi ,Masasi ,Manyoni, Biharamulo na Sumbawanga.
- Mafunzo yalilenga kujenga uwezo wa kuandaa na kuratibu mipango inayozingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu

# Mauaji ya watu wenye Ualbino

- Kutokana na wimbi la mauaji ya watu wenye ualbino nchini  Wizara inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kwa kushirikiana na taasisi za umma na wadau wengine katika kukabiliana na ukatili huu.  Mojawapo ya hatua hizi ni;
- Kufanya maadhimisho ya Siku ya  Watu Wenye Ualbino . Lengo la maadhimisho ni kuhamasisha jamii kuachana na mila potofu dhidi ya watu wenye ulemavu zinazowanyima haki ya kuishi,kushiriki na kulindwa .

# …inaendelea.

- WAUJ kwa kushirikiana na wizara nyingine imeunda timu ya wataalamu ianayoandaa mipango mikakati ya namna ya kushughulikia tatizo hili.
- Kufanya ufuatiliaji wa huduma zinazotolewa katika vituo vinavyolea watoto wenye ualbino
- Kutoa elimu na uhamasishaji kupitia vyombo vya habari na mikutano ya uhamasishaji.

# Hali ya Vituo vya kulelea Watoto Wenye Ualbino

- Vitendo vya Mauaji na ukatili dhidi ya watu wenye ualbino vimelazimisha baadhi ya watoto wenye ualbino kulelewa  katika vituo visivyo rasmi vya kulelea watoto hao hususan katika mikoa ya Kanda ya Ziwa .Baadhi ya Vituo ni Buhangija ,(Shinyanga) Watoto 301(me 156,ke 145) Shule ya Mwisenge (Mara)54(ke 31,me 23)Huruma Children Home 18(ke 14,me 4) Cheyo Children Home 7(me 4,ke 3) Gongoni 7(me 4,ke 3) (Tabora) na Kabanga , Kigoma (72)

# Changamoto katika vituo hivi ;

- Idadi kubwa ya watoto (hususani Buhangija)
- Bajeti ndogo toka serikalini
- Watoto kutotengamanishwa na famila zao
- Wazazi na walezi kutowatembelea watoto.
- Mmomonyoko wa maadili katika vituo .

# Maelekezo ya Wizara

- Maafisa Ustawi wa Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri kufanya ufutiliaji wa wazazi na walezi wa watoto hao ili waweze kuwa karibu na watoto wao.
- Maafisa Ustawi wa Jamii kuvisimamia vituo vinavyolea watoto kuwa na mpango wa malezi (Care plan) ili kuwaunganisha na jamii zao.
- Maafisa Ustawi wa jamii kuhakikisha halmashauri zote zinawatambua watoto wenye ulemavu na na kutunza kumbukumbu zao.

# …Inaendelea.

- Mkoa wa Shinyanga uangalie upya uendeshaji wa Kituo cha Buhangija kwa kuwa pamoja na kuwa ni shule lakini wakati huohuo kinaendeshwa kama makao ya watoto .

# Baraza la ushauri kwa Watu Wenye Ulemavu

- Wizara imezindua Baraza la Ushauri la Taifa kwa Watu Wenye Ulemavu. Majukumu ya Baraza ni pamoja na kushauri kuhusu huduma kwa watu wenye ulemavu.
- Wizara itaandaa taratibu za uanzishaji wa Mabaraza haya katika ngazi za Mikoa , Wilaya , Kata na Mtaa/kijiji.

# Makazi ya Wazee na watu wenye Ulemavu

- Wizara imeendelea kutoa huduma kwa wazee na watu wenye ulemavu katika makazi 17. Kwa mwaka 2014/2015 jumla ya wahudumiwa 896 wamepatiwa huduma muhimu za kujikimu; kama chakula, afya , malazi ,unasihi na utengamao.
- Ili kuboresha huduma katika makazi , Wizara kwa kushirikiana na wadau imeanza kuangalia namna bora ya kuendesha makazi haya.

# Vyuo vya Ufundi na Marekebisho kwa Watu wenye Ulemavu

- Kwa sasa ni vyuo viwili tu vya watu wenye ulemavu vinavyofanya kazi. Chuo cha Singida na Yombo Dar es Salaam.
- Jumla ya watu wenye ulemavu 63 walihitimu mafunzo ambapo wanawake ni 34 na wanaume 29. Jumla ya vijana wenye ulemavu 110 wanaendelea na mafunzo ambapo (ke ) ni 51 na me (59)
- Hata hivyo Vyuo vinne ( 4) havifanyi kazi kutokana na uchakavu wa miundombinu na changamoto ya kibajeti. Juhudi zinaendelea ili kuvihuisha vyuo hivyo.

# Wajibu wa Watalamu wa Afya na Ustawi wa Jamii

- Kuhakikisha Halmashauri zinatenga bajeti ya kutosha ya huduma za Ustawi wa Jamii kama inavyoelekezwa katika miongozo kama CCHP ,miongozo ya bajeti na Sera .
- Sekretarieti za Mikoa kuendelea kusimamia Halmashauri kuomba vibali vya ajira kwa Maafisa ustawi wa Jamii na Maafisa Ustawi Jamii wasaidizi katika ngazi zote.

# …..inaendelea

- Vituo vya kutolea huduma za Afya vihakikishe vinatenga madirisha kwa ajili ya matibabu kwa wazee pamoja na huduma rafiki kwa watoto na watu wazima waliofanyiwa vitendo vya ukatili na unyanyasaji.
- Ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya uzingatie masuala ya ujongeaji kwa watu wenye ulemavu

# HITIMISHO

Ndugu wajumbe kauli mbiu ya mwaka huu ni ***Uwajibikaji wa watumishi wa ngazi zote ndiyo msingi imara katika utoaji wa huduma za afya na ustawi wa jamii zenye ubora unaotakiwa.Ewe mtumishi timiza wajibu wako. Hivyo;*** Wote kwa pamoja tushirikiane kuhakikisha *Kuwa na jamii yenye afya bora na ustawi ambayo itachangia kikamilifu katika maendeleo binafsi na ya nchi.*

# Mwisho



Asanteni